**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)**

**TAARIFA KWA UMMA**

# MATOKEO YA UCHAGUZI WA UDAHILI KUPITIA MFUMO WA UDAHILI WA PAMOJA (CAS) KWA KOZI ZA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linautaarifu umma kuwa matokeo ya uchaguzi wa awamu ya kwanza kwa waombaji wa programu za Afya na Sayansi Shirikishi kwa mwaka wa masomo 2025/2026 yanatangazwa rasmi leo tarehe 25 Julai, 2025.

Baraza liliratibu udahili wa wanafunzi katika kozi mbalimbali za afya na sayansi shirikishi kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (CAS) kwa mwaka wa masomo 2025/2026. Jumla ya waombaji **33,986** waliwasilisha maombi yao kupitia CAS. Jumla ya waombaji **27,785** walikamilisha maombi yao kwa kuchagua vyuo/programu walizozipenda. Jumla ya waombaji **25,515** walikuwa na sifa kwenye programu walizoomba na jumla ya waombaji **2,270** hawakuwa na sifa kwenye programu walizoomba.

Jumla ya waombaji **21,565** wamechaguliwa kujiunga kwenye vyuo vinavyotoa programu mbalimbali za Afya na Sayansi Shirikishi ambapo wanawake **11,013** (51%) na wanaume **10,552** (49%). Waombaji **4,733** walichaguliwa kwenye vyuo vya serikali na waombaji **16,832** katika vyuo visivyo vya serikali.

Aidha, waombaji wenye sifa ambao hawakuchaguliwa kutokana na ushindani katika programu na vyuo walivyoomba, wanashauriwa kuomba kujiunga katika vyuo vyenye nafasi katika dirisha la awamu ya pili kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja.

Waombaji wote wanaweza kuangalia matokeo ya uchaguzi kupitia tovuti ya Baraza (www.nactvet.go.tz) kwa kubonyeza ***CAS Selection 2025*** *kwa ajili ya kupata taarifa zaidi*.

Baraza linautaarifu umma kuwa dirisha la awamu ya pili limefunguliwa rasmi leo tarehe 25/07/2025 hadi tarehe 24/08/2025 na matokeo ya uchaguzi yatatolewa tarehe 01/09/2025.

Aidha, wale wanaohitaji kubadilisha programu au chuo, dirisha la uhamisho litakuwa wazi kuanzia tarehe 25/07/2025 hadi tarehe 24/08/2025, hivyo watumie dirisha hili kukamilisha maombi hayo kupitia tovuti ya Baraza kwa kubonyeza **kwenye akaunti yake aliyotumia kuomba na kuchaguliwa.**

**IMETOLEWA NA:**
**OFISI YA KATIBU MTENDAJI**
**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)**
**25/07/2025**